

La simplicité en Christ

Par Michael Cziesla
des soixante-dix

Unyofu na Usafi kwa Kristo

Na Mzee Michael Cziesla
Wa Sabini

Conférence générale d'octobre 2025

Mettre en pratique la doctrine du Christ de manière simplifiée et ciblée nous aidera à trouver de la joie dans notre vie.

Kutumia mafundisho halisi ya Kristo katika njia iliyorahisishwa na yenye fokasi kutatusaidia sisi kupata shangwe katika maisha yetu ya kila siku.

1. Introduction

Il y a trente-trois ans, j'ai été appelé à servir comme missionnaire dans la mission d'Ogden, en Utah. Naturellement, étant originaire d'Europe, certaines traditions d'Utah, telles que la « gelée verte aux carottes » ou les « pommes de terre funéraires » me paraissaient un peu étranges !

En revanche, j'ai été profondément impressionné par l'exemple de nombreux saints dévoués menant une vie de disciple, par le nombre vertigineux de personnes assistant aux réunions de l'Église et par l'ampleur des programmes de l'Église pleinement opérationnels. À la fin de ma mission, je voulais m'assurer que ma future famille ait accès à cette joie que j'avais ressentie, et à la force et à la maturité spirituelle que j'avais observées. J'étais déterminé à revenir au plus vite mener ma vie à « l'ombre des collines éternelles ».

Cependant, le Seigneur avait d'autres desseins pour moi. Le premier dimanche après mon retour de mission, mon évêque avisé m'a appelé à servir en tant que président des jeunes gens de notre paroisse. En servant ce merveilleux groupe de jeunes gens, j'ai vite compris que la joie que l'on ressent lorsqu'on est disciple du Christ a très peu à voir avec l'affluence aux réunions de l'Église ou l'envergure des programmes.

Ainsi, lorsque j'ai épousé ma merveilleuse femme, Margret, nous avons joyeusement décidé de rester en Europe et d'élever notre famille dans notre pays d'origine, l'Allemagne. Ensem-

1. Utangulizi

Miaka thelathini na mitatu iliyopita nilipokea wito wangu wa kuhudumu kama mmisionari katika Misheni ya Ogden Utah. Hakika, kwa sababu nilikuja kutoka Ulaya, baadhi ya desturi za Utah kama vile “jeli ya kijani na karoti” au “viazi vya matangani” vilikuwa vitu vya kipekee sana!

Hata hivyo, nilifurahishwa sana na moyo wa ibada na uanafunzi wa wengi wa watakatifu, idadi tu iliyokuwa ikihudhuria mikutano ya Kanisa, na kiwango cha ufanyaji kazi kikamilifu cha programu za Kanisa. Wakati misheni yangu ilipofika tamati, nilitaka kuhakikisha kwamba shangwe niliyojisikia na nguvu ya kiroho na ukomavu niliouona vingepatikana pia kwa ajili ya familia yangu ya siku zijazo. Nilikuwa nimeazimia kurudi upesi kuishi maisha yangu katika “vivuli vya vilima vya milele.”

Hata hivyo, Bwana alikuwa na mipango tofauti. Jumapili yangu ya kwanza nyumbani, askofu wangu mwenye hekima aliniita nihudumu kama rais wa Wavulana katika kata yetu. Kuhudumia kundi hili la wavulana wazuri, nilijifunza upesi kwamba shangwe ambayo huja kutokana na kuwa mwanafunzi wa Kristo kwa vyo vyote vile haihusiani na ukubwa wa mikutano ya Kanisa au viwango vya programu.

Kwa hiyo nilipomuoa mke wangu mrembo Margret, kwa shangwe tuliamua kuishi Ulaya na kulea familia yetu katika nchi yetu ya nyumbani ya Ujerumani. Kwa pamoja tulishuhudia kile Rais

ble, nous avons été témoins de la véracité des paroles enseignées par le président Nelson il y a plusieurs années : « La joie que nous ressentons dépend peu de notre situation, mais entièrement de l'orientation de notre vie. » Lorsque notre vie est centrée sur le Christ et sur le message de son Évangile, nous pouvons recevoir la plénitude des bénédictions du disciple, qu'importe l'endroit où nous vivons.

2. La simplicité à l'égard de Christ

Cependant, dans un monde de plus en plus profane, complexe et déroutant, plein d'exigences et de messages différents, et souvent contradictoires, comment pouvons-nous éviter l'aveuglement spirituel et l'endurcissement de notre cœur, tout en restant concentrés sur les « choses claires et précieuses » de l'Évangile de Jésus-Christ? Pendant une période de confusion, l'apôtre Paul a donné un conseil précieux aux saints de Corinthe en leur rappelant de se concentrer sur « la simplicité à l'égard de Christ ».

La doctrine du Christ et la loi de l'Évangile sont si simples que même les petits enfants peuvent les comprendre. Nous pouvons accéder au pouvoir rédempteur de Jésus-Christ et recevoir toutes les bénédictions spirituelles que notre Père céleste a préparées pour nous, en exerçant la foi en Jésus-Christ, en nous repentant, en étant baptisés, en étant sanctifiés par le don du Saint-Esprit et en persévérant jusqu'à la fin. Russell M. Nelson a magnifiquement décrit ce voyage comme étant « le chemin des alliances » et le processus pour devenir « un disciple dévoué de Jésus-Christ ».

Si ce message est si simple, pourquoi semble-t-il souvent si difficile de vivre la loi du Christ et de suivre son exemple ? Il se peut que nous interprétions à tort la simplicité comme quelque chose de facile à atteindre sans effort ni diligence. Suivre le Christ demande des efforts constants et un changement continu. Nous devons nous « dépouille[r] de l'homme naturel [et devenir semblables] à un enfant ». Pour cela, nous devons nous « [confier] en l'Éternel » et nous libérer de la complexité, comme le ferait un petit enfant. Mettre en pratique la doctrine du Christ de manière simplifiée et ciblée nous aidera à trouver de la joie dans notre vie quotidienne, à être

Russell M. Nelson alichofundisha miaka mingi iliyopita “Shangwe tunayojisikia haichangiwi na hali ya maisha yetu na kitu cho chote kinachohusiana na fokasi ya maisha yetu.” Fokasi ya maisha yetu inapokuwa katika Kristo na ujumbe wa injili Yake, tunaweza kupata baraka kamili za uanafunzi mahali po pote tunapoishi.

Unyofu na Usafi Ambao Uko katika Kristo

Hata hivyo, katika ulimwengu ambao unaongezeka kuwa wa kiulimwengu, changamani, na wenye kukanganya, ukiwa na jumbe na matakwa tofauti na mara nyingi kinzani, ni kwa jinsi gani tunaweza kuepukana na macho yetu kupofushwa na mioyo yetu kufanywa iwe migumu na kubaki tumefokasi kwenye “vitu vilivyo wazi na vyenye thamani” vya injili ya Yesu Kristo? Wakati wa mkanganyiko, Mtume Paulo alitoa ushauri mkuu kwa Watakatifu wa Korintho kwa kuwakumbusha wao kufokasi kwenye “unyofu na usafi kwa Kristo.”

Mafundisho ya Kristo na sheria ya injili ni rahisi sana kiasi kwamba hata watoto wadogo wanaweza kuelewa. Tunaweza kupata nguvu za Yesu Kristo za ukombozi na kupokea baraka zote za kiroho Baba wa Mbinguni yetu ameziandaa kwa ajili yetu kwa kufanya imani katika Yesu Kristo, kutubu, kubatizwa, na kupokea kipawa cha Roho Mtakatifu, na kuvumilia hadi mwisho. Rais Nelson alielezea safari hii vizuri sana kama “njia ya agano” na mchakato wa kuwa “mwanafunzi wa Yesu Kristo mwenye kumchamunga.”

Kama ujumbe huu ni rahisi hivyo, kwa nini mara nyingi ionekane kama changamoto kishi sheria ya Kristo na kuufuata mfano Wake? Inaweza kuwa tunafafanua kimakosa unyofu na usafi kama kitu ambacho ni rahisi kukipata bila juhudi au bidii. Kumfuata Kristo kunahitaji juhudi za kila mara na mabadiliko endelevu. Tuna-hitaji “[kumvua] mtu wa asili na ... [kuwa kama mtoto] mdogo.” Hii hujumuisha kuweka “tumaini letu kwa Bwana” na kuacha uchangamani kuondoka, kama vile tu watoto wadogo wanavyofanya. Kutumia mafundisho ya Kristo katika njia iliyorahisishwa na yenye fokasi kutatusaidia sisi kupata shangwe katika maisha yetu ya kila siku, kutupa

guidés dans nos appels, à répondre à certaines des questions les plus complexes de la vie et à trouver la force de faire face à nos plus grands défis.

Mais comment pouvons-nous intégrer concrètement cette simplicité dans notre vie de disciples du Christ, tout au long de notre existence ? Le président Nelson nous a rappelé de nous concentrer sur « la vérité pure, la doctrine pure et la révélation pure » tandis que nous nous efforçons de suivre le Sauveur. Le fait de se demander régulièrement : « Qu'est-ce que le Seigneur Jésus-Christ voudrait que je fasse ? » ouvre la voie à des directives profondes. En suivant son exemple, nous trouvons un chemin sûr à travers l'incertitude, et une main aimante et directrice à tenir jour après jour. Il est le Prince de la paix et le Bon Berger. Il est notre Consolateur et notre Libérateur. Il est notre Rocher et notre Refuge. C'est un ami : le vôtre et le mien ! Il nous invite tous à aimer Dieu, à respecter ses commandements et à aimer notre prochain.

Lorsque nous choisissons de suivre son exemple, d'aller de l'avant avec foi en lui, d'accepter pleinement le pouvoir de son Expiation et de nous souvenir de nos alliances, l'amour remplit notre cœur, l'espérance et la guérison élèvent notre esprit, et l'amertume et le chagrin font place à la gratitude et à la patience d'attendre les bénédictions promises. Parfois, nous devons nous éloigner d'une situation malsaine ou nous faire aider par un professionnel. Mais dans tous les cas, la mise en pratique des principes simples de l'Évangile nous permet de surmonter les difficultés de la vie à la manière du Seigneur.

Nous sous-estimons parfois la force que nous recevons d'actes simples, comme prier, jeûner, étudier les Écritures, nous repentir quotidiennement, prendre la Sainte-Cène chaque semaine et adorer régulièrement dans la maison du Seigneur. Mais, quand nous réalisons qu'il n'est pas nécessaire de faire « quelque chose de difficile » et que nous nous concentrons sur la mise en pratique de la doctrine pure et simple, nous commençons à voir que l'Évangile nous « est merveilleusement bénéfique », même dans les situations les plus difficiles. Nous trouvons de la force et de « l'assurance devant Dieu », même au cœur de nos souffrances. M. Russell Ballard nous a souvent rappelé que « c'est dans cette simplicité que [nous trouverons] la paix, la joie et le bonheur ».

La mise en application de la simplicité qui

mwongozo katika miito yetu, kujibu baadhi ya maswali changamani sana ya maisha, na kutoa nguvu za kukabiliana na changamoto zetu kubwa sana.

Lakini ni kwa jinsi gani sisi kiutendaji tunatelekeza hili kwa urahisi katika safari yetu ya maisha yote kama wanafunzi wa Kristo? Rais Nelson alitukumbusha tufokasi kwenye “ukweli halisi, mafundisho safi, na ufunuo halisi” tunapotafuta kumfuata Mwokozi. Mara kwa mara tukiuliza, “Ni nini Bwana Yesu Kristo angetaka nifanye? kuna funua mwelekeo muhimu. Kufuata mfano Wake kunatoa njia salama kupitia kutokuwa na uhakikana mkono wenye upendo, wenye kuongoza ili tuushikilie siku hadi siku. Yeye ni Mfalme wa Amani na Mchungaji Mwema. Yeye ni Mfariji na Mkombozi Wetu. Yeye ni Mwamba na Kimbilio Letu. Yeye ni Rafiki—rafiki yako na rafiki yangu! Yeye anatalika sisi sote kumpenda Mungu, kushika amri Zake, na kumpenda jirani yetu.

Tunapochagua kufuata mfano Wake na kusonga mbele kwa imani katika Kristo, kukumbatia nguvu ya Upatanisho Wake na kukumbuka maagano yetu, upendo hujaza mioyo yetu, tumaini na uponyaji vinainua roho zetu, na machungu na huzuni vinabadilishwa na shukrani na subira ya kusubiria baraka zilizohidiwa. Wakati mwingine, tunaweza kuhitaji kujitenga mbali wenyewe kutoka kwenye hali zisizo nzuri na kutafuta msaada wa kitaalamu. Lakini katika kila hali, kutumia kanuni rahisi za injili kutatusaidia kupita changamoto za maisha katika njia ya Bwana.

Wakati mwingine tunapuuza nguvu tunayopokea kutokana na vitendo rahisi kama sala, kufunga, kujifunza maandiko, toba ya kila siku, kupokea sakramenti kila wiki, na kuabudu kila mara katika nyumba ya Bwana. Lakini tunapotambua kwamba hatuhitaji “kufanya vitu vikubwa” na kujikita wenyewe kwenye kutumia mafundisho halisi na rahisi, tunaanza kuona jinsi injili “inavyofanya kazi ya kushangaza” kwa ajili yetu, hata katika mazingira yenye changamoto sana. Tutapata nguvu na “kujiadini mbele za Mungu,” hata wakati tunapatwa na machungu. Mzee M. Russell Ballard alitukumbusha sisi mara nyingi, “Ni katika urahisi huo ambapo [sisi] tutapata ... amani, shangwe, na furaha.”

Kutumia unyofu na usafi ambao upo ka-

est en Christ nous pousse à donner la priorité aux personnes plutôt qu'aux processus et aux relations éternelles plutôt qu'aux comportements à court terme. Au lieu de nous laisser absorber par l'aspect logistique de notre service, nous nous concentrons sur « les choses qui importent le plus » dans l'œuvre de Dieu pour le salut et l'exaltation. Nous nous libérons pour donner la priorité à ce sur quoi nous pouvons agir, au lieu d'être accablés par ce qui est hors de notre contrôle. Le Seigneur a dit : « C'est pourquoi, ne vous lassez pas de bien faire, car vous posez les fondements d'une grande œuvre. Et c'est des petites choses que sort ce qui est grand. » Quel encouragement puissant à agir avec simplicité et humilité, quelle que soit notre situation.

3. Oma Cziesla

Ma grand-mère, Marta Cziesla, était un merveilleux exemple de personne qui fait « des choses petites et simples » pour que de grandes choses soient réalisées. Nous l'appelions affectueusement Oma Cziesla. Oma a accepté l'Évangile le 30 mai 1926, dans le petit village de Selbongen, en Prusse orientale, avec mon arrière-grand-mère.

Marta Cziesla (à droite) le jour de son baptême.

Elle aimait le Seigneur et son Évangile, et elle était déterminée à respecter les alliances qu'elle avait contractées. En 1930, elle a épousé mon grand-père, qui n'était pas membre de l'Église. À ce moment-là, il est devenu impossible pour Oma d'assister aux réunions de l'Église, car la ferme de mon grand-père était très éloignée de l'assemblée la plus proche. Mais elle s'est concentrée sur ce qu'elle pouvait faire. Oma a continué de prier, de lire les Écritures et de chanter les cantiques de Sion.

Certaines personnes ont peut-être pensé qu'elle n'était plus pratiquante, mais c'était loin d'être le cas. Lorsque ma tante et mon père sont nés, sans détenteur de la prêtrise à la maison, sans réunions de l'Église ni accès aux ordonnances à proximité, elle a de nouveau fait ce qu'elle pouvait et s'est attachée à enseigner à ses enfants « à prier et à marcher en droiture devant le Seigneur ». Elle leur lisait les Écritures, chantait avec eux les cantiques de Sion et, bien sûr, priait avec eux, chaque jour. Une expérience de l'Église appliquée au foyer à 100 %.

tika Kristo hutufanya sisi kuweka kipaumbele kwa watu badala ya michakato na uhusiano wa milele badala ya tabia za muda mfupi. Tunafokasi kwenye “vitu ambavyo vina maana zaidi” katika kazi ya Mungu ya Wokovu na kuinuliwa badala ya kutekwa katika kusimamia utumishi wetu. Tunajiweka wenyewe huru ili kuvipa vipaumbele vitu ambavyo sisitunawezakufanya badala kulemewa na vitutusivyowezakufanya. Bwana alitukumbusha: “Kwa hiyo, msichoke kutenda mema, kwa kuwa mnajenga misingi ya kazi kubwa. Na kutokana na mambo madogo huja yale yaliyo makuu.” Ni himizo lililoje la kutenda katika urahisi na unyenyekevu, bila kujali hali zetu.

3. Oma Cziesla

Bibi yangu Maria Cziesla alikuwa mfano wa kupendeza wa kufanya “mambo madogo na rahisi” ili kuwezesha mambo makuu. Kwa upendo sisi tulimwita Oma Cziesla. Oma alikumbatia injili katika kijiji kidogo cha Selbongen katika East Prussia pamoja na bibi wa mama yangu mnamo Mei 30, 1926.

Marta Cziesla (kulia) katika siku ya ubatizo wake.

Alimpenda Bwana na injili Yake na alikuwa ameazimia kuyashika maagano aliyokuwa amefanya. Katika mwaka wa 1930 aliolewa na babu yangu, ambaye hakuwa muumini wa Kanisa. Wakati fulani ilikuwa vigumu kwa Oma kuhudhuria mikutano ya Kanisa kwa sababu shamba la babu yangu lilikuwa mbali sana kutoka kwenye mkusanyiko uliokuwa karibu zaidi. Lakini yeye alifokasi juu ya kile ambacho angeweza kufanya. Oma aliendelea kusali, kusoma maandiko, na kuimba nyimbo za Sayuni.

Baadhi ya watu wangepikiria yeye hakuwa hai katika imani yake, lakini hilo lilikuwa mbali sana na ukweli. Wakati shangazi yangu na baba yangu walipozaliwa, kukiwa hakuna ukuhani katika nyumba ile na hakuna mikutano ya Kanisa au ufikiaji wa ibada karibu, yeye tena alifanya kile ambacho angeweza kufanya na kufokasi kwenye kuwafundisha watoto wake “kusali, na kutembea wima mbele za Bwana.” Aliwasomea kutoka kwenye maandiko, akaimba pamoja nao nyimbo za Sayuni, na hakika alisali pamoja nao—kila siku. Asilimia 100 ya uzoefu wa nyumba iliyo kitovu cha Kanisa.

En 1945, mon grand-père servait dans l'armée, loin de chez lui. Lorsque l'ennemi s'est approché de leur ferme, Oma a pris ses deux enfants et a quitté leur foyer bien-aimé pour chercher refuge dans un endroit plus sûr. Après un voyage difficile et dangereux, ils ont finalement trouvé refuge dans le nord de l'Allemagne, en mai 1945. Ils n'avaient plus rien, à l'exception des vêtements qu'ils portaient. Mais Oma a continué de faire ce qu'elle était capable de faire : elle priait avec ses enfants, tous les jours. Elle chantait avec eux les cantiques de Sion, qu'elle connaissait par cœur, tous les jours.

La vie était extrêmement difficile et, pendant de nombreuses années, leur principal souci était de pouvoir se nourrir. Puis, en 1955, mon père, alors âgé de 17 ans, est entré dans une école professionnelle dans la ville de Rendsburg. En passant devant un bâtiment, il a vu une petite pancarte à l'extérieur qui disait : « Kirche Jesu Christi der Heiligen der Letzten Tage » — « L'Église de Jésus-Christ des Saints des Derniers Jours ». Il s'est dit : « C'est intéressant, c'est l'Église de maman. » Alors, en rentrant chez lui, il a dit à Oma qu'il avait trouvé son Église.

Vous pouvez imaginer ce qu'elle a dû ressentir après presque vingt-cinq ans sans contact avec l'Église. Elle était déterminée à y assister le dimanche suivant et a convaincu mon père de l'accompagner. Rendsburg se trouvait à plus de 30 kilomètres du petit village où ils vivaient. Mais Oma n'allait pas laisser cela l'empêcher d'aller à l'église. Le dimanche suivant, elle est montée sur son vélo avec mon père, et ils sont allés à l'église.

Lorsque la réunion de Sainte-Cène a commencé, mon père s'est assis au dernier rang, espérant que cela se terminerait rapidement. C'était l'Église d'Oma, pas la sienne. Ce qu'il voyait n'était pas très encourageant : une assemblée constituée de quelques femmes âgées et de deux jeunes missionnaires qui dirigeaient toute la réunion. Mais ils ont commencé à chanter et ils ont chanté les cantiques de Sion que mon père avait entendus depuis tout petit : « Venez, venez, sans craindre le devoir », « Ô mon Père », « Au grand prophète ». En entendant ce petit groupe chanter les cantiques de Sion qu'il connaissait depuis son enfance, son cœur a été touché, et il a su immédiatement et sans l'ombre d'un doute que

Mwaka 1945 babu yangu alikuwa akihudumu katika vita mbali sana na nyumbani. Wakati maadui walipokaribia shamba lao, Oma aliwatwaa watoto wake wawili wadogo na kuliacha shamba walilolipenda na kwenda kutafuta kimbilio katika sehemu salama. Baada ya safari ngumu na ya kutishia maisha, mwishowe walipata kimbilio katika mwezi Mei 1945 huko kaskazini mwa Ujerumani. Hawakuwa na cho chote kilichobaki isipokuwa nguo kwenye miili yao. Lakini Oma aliendelea na kile alichoweza kufanya; alisali pamoja na watoto wake. Aliimba pamoja nao nyimbo za Sayuni alizokuwa amezikariri moyoni—kila siku.

Maisha yalikuwa magumu sana na kwa miaka mingi alifokasi tu katika kuhakikisha kulikuwa na chakula mezani. Lakini mwaka 1955 baba yangu, wakati huo akiwa na umri wa miaka 17, alikuwa anahudhuria shule ya ufundi katika mji wa Rendsburg. Akitembea karibu na jengo aliona ubao mdogo nje ambao umeandikwa “Kirche Jesu Christi der Heiligen der Letzten Tage” — “Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho.” Alifikiria, “Hiyo inapendeza; hili ni Kanisa la mama.” Kwa hiyo alipofika nyumbani, alimwambia Oma kwamba alikuwa amelipata kanisa lake.

Unaweza kufikira jinsi yeye alivyojisikia baada ya karibu miaka 25 ya kutokuwa na mawasiliano na Kanisa. Aliamua kuhudhuria Jumapili iliyofuata na kumshawishi baba yangu kuandamana naye. Rendsburg ilikuwa zaidi ya maili 20 (kilomita 32) kutoka kwenye kijiji kidogo pale walipoishi. Lakini hili halingemzua Oma kuhudhuria Kanisa. Jumapili iliyofuata, alipanda baiskeli yake pamoja na baba yangu na wakaenda kanisani.

Wakati mkutano wa sakramenti ulipoanza, baba yangu alikaa chini katika safu ya mwisho, akitumainia ingeisha punde. Hili lilikuwa kanisa la Oma na si lake. Kile alichokiona hakikupendeza sana: wanawake wakubwa wachache wakihudhuria na wamisionari vijana wawili ambao kwa ufanisi waliendesha kila kitu katika mkutano ule. Lakini kisha walianza kuimba, na waliimba nyimbo za Sayuni ambazo baba yangu alikuwa amezisikia tangu akiwa mvulana mdogo: “Njoo, Enyi, Watakatifu,” “Baba Yangu,” “Sifa kwa Aliyenena na Bwana.” Kulisikia hili kundi dogo likiimba nyimbo za Sayuni alizozijua tangu utotoni kulichoma moyo wake, na yeye alijua mara moja na bila shaka kwamba Kanisa lilikuwa

l'Église était vraie.

La première réunion de Sainte-Cène à laquelle ma grand-mère a assisté après vingt-cinq ans est aussi celle où mon père a reçu une confirmation personnelle de la véracité de l'Évangile rétabli de Jésus-Christ. Il s'est fait baptiser trois semaines plus tard, le 25 septembre 1955, avec mon grand-père et ma tante.

Plus de soixante-dix ans se sont écoulés depuis cette petite réunion de Sainte-Cène à Rendsburg. Je pense souvent à Oma, à ce qu'elle devait ressentir pendant ces nuits solitaires, faisant les petites choses simples qu'elle pouvait faire, comme prier, lire et chanter. Alors que je me tiens ici aujourd'hui à la conférence générale et que je parle de ma grand-mère, mon cœur est rempli d'humilité et de gratitude pour sa détermination à respecter ses alliances et à faire confiance au Seigneur malgré ses épreuves. Je suis touché, non seulement par son exemple, mais aussi par celui de merveilleux saints dans le monde qui, dans leurs situations personnelles difficiles, se concentrent sur la simplicité en Christ, voyant peut-être peu de changement maintenant, mais ayant confiance que de grandes choses arriveront un jour futur.

4. Les choses petites et simples

J'ai appris, par expérience personnelle, que les choses petites et simples de l'Évangile, et le fait de nous concentrer fidèlement sur le Christ nous conduisent à la vraie joie, permettent à de puissants miracles de se réaliser et nous donnent la confiance que toutes les bénédictions promises s'accompliront. C'est aussi vrai pour vous que pour moi. Comme l'a dit Jeffrey R. Holland : « Certaines bénédictions se manifestent rapidement, d'autres tardivement, certaines uniquement aux cieux, mais pour ceux qui embrassent l'Évangile de Jésus Christ, elles se manifestent. » J'en témoigne au nom de Jésus-Christ. Amen.

la kweli.

Mkutano wa kwanza wa sakramenti ambao bibi yangu alihudhuria baada ya miaka 25 ulikuwa ndio mkutano ambao baba yangu alipokea uthibitisho binafsi juu ya ukweli wa urejesho wa injili ya Yesu Kristo. Alibatizwa wiki tatu baadaye, mnamo Septemba 25, 1955, pamoja na babu yangu na shangazi yangu.

Imekuwa miaka zaidi ya 70 tangu huo mkutano wa sakramenti mdogo huko Rendsburg. Mara kwa mara ninafikiria kuhusu Oma, jinsi yeye alivyojisikia katika usiku wa upweke wa siku zile, akifanya vitu vidogo na rahisi alivyoweza kufanya, kama kusali, kusoma na kuimba. Ninaposimama hapa leo katika mkutano mkuu na kuzungumza kuhusu Oma wangu, maamuzi yake ya kushika maagano yake na kumwamini Bwana licha ya mapambano yanaujaza moyo wangu kwa unyenyekevu na shukrani—si tu kwa ajili yake pekee bali kwa wengi wa Watakatifu wa kupendeza kote ulimwenguni ambao wanafokasi kwenye unyofu na usafi kwa Kristo katika hali zao zenye changamoto, pengine kuona mabadiliko kidogo sasa lakini kutumainia kwamba mambo makubwa yatatokea siku nyingine katika siku zijazo.

4. Vitu Vidogo na Rahisi

Nimejifunza kupitia uzoefu wangu mwenyewe kwamba vitu vidogo na rahisi vya injili na kufokasi kwa uaminifu katika Kristo hutuongoza kwenye shangwe ya kweli, vikileta miujiza mikubwa, na hutupatia kujiamini kwamba baraka zote zilizoahidiwa zitakuja. Hii ni kweli kwa ajili yako kama ilivyo kweli kwangu. Katika maneno ya Mzee Jeffrey R. Holland, “Baraka zingine huja haraka, zingine hucheleva, na zingine haziji hadi tufikapo mbinguni; lakini kwa wale wanaokumbatia injili ya Yesu Kristo, zinakuja.” Juu ya hili pia ninashuhudia katika jina la Yesu Kristo, amina.